



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA AFYA

MFUKO WA TAIFA WA BIMA YA AFYA



Unapojibu tafadhali taja;  
Kumb Na:DA.09/219/01A/53

Tarehe: 08 Februari 2023

Wakuu wa Vyuo Vikuu Wote,  
Wakuu wa Vyuo vya Kati Wote,  
Wakuu wa Vyuo vya ufundi Wote  
Tanzania Bara na Zanzibar

**YAH: KUWASILISHA NAMBA ZA UTAIFA (NIN) ZA WANAFUNZI WA VYUO KWA AJILI YA UTAMBUZI KATIKA VITUO VYA KUTOLEA HUDUMA ZA AFYA VILIVYOSAJILIWA NA MFUKO WA TAIFA WA BIMA YA AFYA**

Tafadhali rejea somo tajwa hapo juu.

2. Katika kuhakikisha kwamba wanafunzi wa Vyuo vya Elimu ya Juu na Vyuo vya Kati vilivyosajiliwa na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya wanatambuliwa kwa usahihi wakati wa kupata huduma za matibabu kama inavyokusudiwa na Serikali, Mfuko unaendelea kuimarisha mfumo yake ya TEHAMA ya utambuzi na uhakiki kwa wanufaika wake wanaohitaji kupata huduma za matibabu katika Vituo vya kutolea huduma za afya nchini.
3. Ili kuepuka usumbufu unaoweza kujitokeza kwa wanafunzi wa Vyuo watakapohitaji huduma za matibabu katika vituo vya kutolea huduma vilivyosajiliwa na Mfuko nchini, Chuo chako kinashauriwa kukusanya Namba za Utaifa (NIN) kutoka kwa wanafunzi wote waliolipia au watakaolipia mchango wa bima ya afya na kuwasilisha taarifa hizo katika Ofisi za NHIF za mkoa husika na Ofisi ya Uratibu Zanzibar kwa hatua zaidi.
4. Hivyo, kutokana na umuhimu wa suala hili, tayari Mfuko umeimarisha mfumo wake wa utambuzi wa wanachama katika vituo vya huduma za afya na hivyo umepanga kuanzia tarehe **1.04.2023** utambuzi wa wanachama ikiwemo kundi la wanafunzi watakaohitaji huduma za matibabu utafanyika kwa kutumia alama za vidole (Biometric Finger Print Identification). Jedwali la uwasilishaji wa taarifa zinazotakiwa kuwasilishwa na Chuo katika Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya limeambatishwa kwa rejea wakati wa utekelezaji.
5. Tunashukuru kwa ushirikiano wako wa dhati

Mapunda C, G.  
Kny. **MKURUGENZI MKUU**

**Nakala:** Meneja wa Mkoa,  
Meneja Ofisi ya Uratibu Zanzibar

**JEDWALI LA UWASILISHAJI WA TAARIFA ZA NAMBA ZA UTAMBULISHO KWA  
WANAFUNZI WA VYUO VIKUU NA VYUO VYA KATI**

| AdmissionNo | FormFourIndexNo | NationalIdentificationNo | StudentFullName |
|-------------|-----------------|--------------------------|-----------------|
|             |                 |                          |                 |
|             |                 |                          |                 |
|             |                 |                          |                 |
|             |                 |                          |                 |
|             |                 |                          |                 |
|             |                 |                          |                 |
|             |                 |                          |                 |